# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA
# MTIHANI WA KUHITIMU KIDATO CHA SITA

**121/1** **KISWAHILI 1**

(Kwa watahiniwa Walioko na Wasiokuwa Shuleni)

**Muda: Saa 3:00** **Mwaka: 2023**

**Maelekezo**

1. Karatasi hii ina sehemu A na B zenye jumla ya maswali **nane (8)**.
2. Jibu maswali yote katika sehemu A na maswali **matatu (3)** kutoka sehemu B. Swali la **sita (6)** ni la lazima.
3. Sehemu A ina alama **arobaini (40)** na sehemu B ina alama **sitini (60)**.
4. Zingatia maagizo ya **kila sehemu** na ya **kila swali**.
5. Majibu yote yaandikwe kwa kalamu yenye wino wa **bluu** au **mweusi**.
6. Simu za mkononi na vitu vyote visivyoruhusiwa **havitakiwi** katika chumba cha mtihani.
7. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

## SEHEMU A (Alama 40)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

1. Soma kifungu cha habari kifuatacho kwa makini kisha jibu maswali yanayofuata:

Mfumo wa elimu ya kikoloni ulichangia sana kuua sanaa za jadi. Watoto wengi walikwenda katika shule zilizoendeshwa na wamisheni walioamini kuwa, mtanzania lazima atupilie mbali utamaduni wake. Kwa hiyo walihakikisha kuwa wanalea watoto wa kitanzania katika hali ambayo hawakushirikishwa katika vipengele fulani vya maisha yao ya kijadi hasa vile vya sanaa za maonyesho za jadi. Shule nyingi za bweni ziliwakataza wanafunzi kushiriki au kutazama ngoma za asili. Ilikuwa rahisi kuwatenganisha wanafunzi hawa na sanaa za maonyesho za jadi kwa vile shule nyingi wakati huo ziliwapa wanafunzi muda mchache wa kuwa nyumbani. Kipindi wawapo likizo kulikuwa na jopo maalumu la kuangalia mienendo ya wanafunzi hao na kuhakikisha kuwa hawashiriki katika mambo ya jadi.

Mwisho wa muhula kabla ya kwenda likizo, wahisani waliomiliki shule hizo, walikuwa wanawahubiria na kuwasisitiza wanafunzi pindi wawapo likizo wasishiriki katika ngoma, unyago na matambiko kwa kuwa ni ushetani kushiriki katika sanaa hizo. Aidha, wanafunzi walisisitizwa kuelimisha jamii zao kuwa shughuli hizo ni ushetani hivyo waachane nazo kabisa.

Pamoja na athari nyingine zilizotokana na mfumo huo wa elimu ambao pia ulilenga katika kuwafanya watanzania wazungu weusi, kizazi kipya cha Tanzania kilikuwa katika hali ya kuamini kuwa ilipaswa kuachilia mbali mila na desturi za kitanzania. Katika kutekeleza imani hiyo, sanaa za maonyesho za jadi zilikuwa kitu kimojawapo kilichotupiliwa mbali.

Wanafunzi walianza kufundishwa sanaa za maonyesho mamboleo, yaani drama. Waliipokea sanaa hii mpya kwa mikono miwili, hasa kwa vile hawakuwa na kingine chochote badala yake. Katika hali hiyo walikuwa wakiamini kuwa, sanaa za maonyesho si kitu kingine zaidi ya drama kama ilivyoletwa na wazungu na vichekesho vilivyotokana na drama hiyo. Halikuwajia wazo kuwa zile ngoma, majigambo, miviga na utambaji hadithi vitu ambavyo walikuwa wanazotupilia mbali ndivyo hasa vilivyokuwa sanaa za maonyesho za utamaduni wao.

Jambo hili bado ni tatizo kubwa hadi leo katika uwanja wa sanaa za maonyesho. Kuna ubishi mkubwa kuhusu suala la sanaa za maonyesho za kiafrika. Wapo wanaosema kuwa hakuna sanaa za maonyesha za kiafrika na wapo wanaosema zilikuwepo kabla ya wageni na bado zipo. Ukweli ni kwamba watu sasa wamegutuka na wanajaribu kutafakari kama ule uamuzi wao wa kutupilia mbali vipengele kadhaa vya utamaduni wao ulikuwa sahihi.

Kulikuwapo wachache katika jamii waliokuwa na ujasiri na kukubali kuitwa washamba na washenzi. Hawa hawakuwa tayari kutupilia mbali kitu ambacho waliamini ndicho kilichosaidia kujenga utu wao na jamii. Wengi kati ya hao ni watanzania walioishi vijijini

ambao hawakuathiriwa sana na ustaarabu wa kigeni na ndio waliowezesha Tanzania ya leo kuwa na ngoma, majigambo na utambaji hadithi wa kitanzania.

**Maswali**

(a) Kwa kutumia maneno yasiyozidi matano andika kichwa cha habari uliyosoma.

(b) Kwa nini wanafunzi walizuiliwa kushiriki katika mambo ya jadi wakati wa enzi za ukoloni? Bainisha sababu mbili.

(c) Fafanua maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika habari hii:
   (i) Wamisheni
   (ii) Wahisani
   (iii) Wamegutuka
   (iv) Wazungu weusi

(d) Kwa kutumia maneno yasiyopungua ishirini, fafanua wazo kuu la mwandishi linalopatikana katika aya ya nne.

2. (a) Kuna tofauti gani kati ya nafsi na viambishi viwakilishi vya nafsi katika kitenzi? Tumia hoja sita katika ufafanuzi wako.

   (b) Eleza kwa mifano, dhima nne za viambishi katika kitenzi cha Kiswahili.

3. Andika vitenzi vifuatavyo katika kauli zilizowekwa kwenye mabano kisha bainisha viambishi vya kauli husika.

   (a) Panga (Kutendesha)
   (b) Piga (Kutendeana)
   (c) Saidia (Kutendana)
   (d) Choma (Kutendewa)

4. Lugha ya kuzungumza na lugha ya kuandika zinatumika kufikisha ujumbe kwa hadhira ingawa zinatofautiana. Kwa kutumia mifano, fafanua mambo matano kudhihirisha tofauti hizo.

**SEHEMU B (Alama 60)**

Jibu maswali **matatu (3)** katoka sehemu hii. Swali la **sita (6)** ni la lazima.

5. Andika insha ya maneno yasiyozidi mia nne (400) na yasiyopungua mia tatu hamsini (350) kuhusu ujangili nchini Tanzania.

6. Juma amepewa kazi ya kutafsiri matini iliyoandikwa kwa Lugha ya Kiswahili kwenda Lugha ya Kiingereza. Eleza mbinu nne anazoweza kuzitumia kufanya kazi hiyo.



csee2023

7. "Lugha ya Kiswahili inatumika katika shughuli mbalimbali barani Afrika na ulimwenguni kwa ujumla." Kwa kutumia hoja sita, thibitisha kauli hiyo kwa mifano.

8. Eleza majukumu ya TAKILUKI na Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima katika kukuza lugha ya Kiswahili nchini Tanzania. Tumia hoja tatu kwa TAKILUKI na hoja tatu kwa Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima.



«see2023